

Pambazuko

Toleo Namba 027

Jumatatu Januari 16-22, 2023



Manusura Precision kuambulia milioni 70/-

Uk. 10

DCI, DPP washtakiwa

● *Yatakiwa itamkwe 'wameshindwa kazi'*

Samia akarabati mwavuli wa siasa



Uk. 11

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Samia kemea wanaokuharibia

RAIS wa Tanzania Samia Rusuluu Hassan mpaka sasa akiwa anakaribia kufikisha miaka miwili akiwa madarakani, anathibitisha kwamba anaweza kufanya vyema zaidi katika utendaji wake wa kazi ya kuongoza nchi, lakini huenda imani ya wananchi wake ikafifia ikiwa ataendelea kukaa kimya bila kukemea wenye kutaka “kumharibia.”

Wenye kutaka kumharibia Rais Samia wapo wengi; miongoni mwao ni watendaji wabovu katika ofisi za kutoa huduma kwa wananchi, hasa za serikali, halmashauri na kwenye taasisi za umma ambako wananchi wanapaswa kuhudumiwa vyema.

Katika ofisi nyingi za kutoa huduma kwa wananchi, sasa zimekuwa na watendaji wengi wa hovyoy, wavivu, wanatumia muda na rasilimali za serikali kufanya mambo yao binafsi.

Pambazuko limepokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi ambao wanahoji – “kulikoni?” Kwamba nini kimetokea hadi watendaji waliokuwa na nidhamu ya kazi, kuwajibika, kujituma na kuhudumia vyema wateja wao-wananchi, sasa wamebadilika!

Mbali na kuwajibika ipasavyo, malalamiko hayo mengine yanadai kuwepo ongezeko la rushwa, kwamba watendaji wengi wa serikali sasa hawana woga wa kuomba rushwa ili kutoa huduma kwa wananchi.

Je, nani amewaambia kuwa Rais Samia ni mpole kiasi cha kufumbia ujinga huo wa kudai rushwa kana kwamba ni haki yao kabla ya kutoa huduma, tena nyingine zikiwa bure kabisa!

Wapo wanaoenda mbali zaidi

na kueleza kwamba huenda kauli ya Rais Samia kwamba “kila mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake,” umechukuliwa kama ruhusa ya kuikumbatia rushwa?

Sisi katika Pambazuko hatuamini kauli hiyo ya Rais Samia kama ilikuwa ni fursa ya kuruhusu watendaji wa serikali kuitumia kuomba rushwa ili kutoa huduma kwa wananchi.

Tunaamini tu kwamba wanaoichukua kauli hiyo kuwa ruksa, ni wale wenye hulka ya rushwa na kamwe siyo msukumo wa kauli hiyo unaowafanya kuomba rushwa kana kwamba ni haki yao ya msingi kabla ya kutoa huduma kwa wananchi.

Kikubwa ambacho Rais Samia anapaswa kujiepusha nacho, ni kuhakikisha kuwa wasaidizi wake anawafuatilia kwa karibu kwa kutumia vyombo vyake vingi; vya wazi na hata vile vya sirini ili kuhakikisha wale wote wenye lengo la “kumharibia” wanajulikana na kudhibitiwa mapema kabla madhara hayajawa makubwa au kuota mizizi.

Madhara ya watendaji wavivu na wala rushwa yanajulikana kwani huwakosesha wananchi haki zao za kupata huduma kutoka ofisi za serikali na kugeuza lawama zote kwa kiongozi wa nchi, ambaye sasa ni Rais Samia.

Kuwadhibiti wote wenye malengo mabaya, hata kama wao binafsi wanatajirika kwa rushwa na wizi mwingine, ni kazi inayopaswa kuimarishwa sasa na kuwa endelevu ili kujenga Tanzania ambayo itakuwa nchi ya kupigiwa mfano kwa kutokuwa na rushwa na kuwepo kwa watendaji wa serikali wenye weledi na ufanisi mkubwa.



Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



*“Mwalimu anaweza kufundisha bila darasa, lakini darasa haliwezi kufanya kitu chochote bila mwalimu. Baada ya kuweka madarasa mengi nguvu kubwa sasa iwekwe kwa walimu ili kuwe na uwiano kati yao na wanafunzi na madarasa
- Richard Mabala, mwalimu na mwanaharakati wa elimu bora Tanzania.*

Katiba ni jicho la ubinadamu

Na Tryruckia MFINANGA

KATIKA ukurasa wa tisa, katika gazeti hili, toleo namba 2, Evarist Chahali aliandika makala yenye kichwa cha maneno, “Nasubiri muujiza kuheshimu Katiba Mpya.”

Lengo lake lilikuwa ni “kuamsha tafakuri” kuhusu swali lifuatalo; “Kama Katiba iliyopo inapuuza, miujiza gani itakayowezesha Katiba mpya (yenye kukataza tabia mbaya kama vile wizi, uwongo, ujambazi na kuminya haki za binadamu) kuheshimiwa?”

Nimeamua kuchangia kimawazo kwenye mjadala huu kwa sababu ya umuhimu wake katika kazi ya kujenga “imani ya jamii” inayotwezesha kujenga “jamii ya amani.”

Nitajibu swali la Chahali katika hatua mbili. Kwanza ni maelezo kuhusu nafasi ya sheria na Katiba katika jamii. Na pili, ni ufafanuzi wa kuondoa utata wa kimisamiati.

Kuhusu Katiba na sheria napenda kusema kwamba, kama watu wote wangukuwa na afya njema, basi tusingehitaji madaktari wanaotoa huduma za “tiba ya kiafya” kwa wagonjwa pekee.

Vivyo hivyo, “tiba ya kisheria” inawahusu watu wenye hulka ya uhalifu. Na kimaumbile wanadamu wote wanayo hulka ya uhalifu.

Tunafahamu kuwa, kwa maumbile yake, kila binadamu ni kitovu cha fikra, uamuzi na matendo huru ya kimwili. Anayo hiari ya kuchagua kati ya malengo mema na malengo mabaya.

Lakini, ulinzi wa maslahi ya pamoja katika jamii, hauruhusu uhiari kama huo. Maslahi ya pamoja ni muhimu kuliko maslahi binafsi. Hivyo, tunahitaji Katiba na sheria zinazotamka adhabu kwa wakiukaji.

Katiba ya nchi na sheria za Bunge ni walimu wazuri katika eneo hili, hata kama watachalewa kuingia darasani au watafundisha bila kueleweka kwa



Hawa wanadai Katiba Mpya

wanafunzi wengi. Kwa hiyo, Katiba na sheria haviepukiki katika jamii.

Sasa nijielekeze katika swali la kimisamiati. Chahali aliongela tabia mbaya kama vile wizi, uwongo, ujambazi, na ukiukwaji wa haki za binadamu.”

Kimsingi, kiongozi yeyote mwadilifu ahitaji kuwepo kwa Katiba mpya ili ajue ama kufuata utu kwamba wizi, rushwa, uongo na makatazo mengine ni tabia mbaya na haifai.

Katiba na sheria zinakuwepo kwa kuwa kila binadamu; hata viongozi wakubwa kabisa na wenye heshima, wanaweza kukumbatia uongo, wizi, rushwa, kuonea na kunyanyasa watu bila sababu za msingi, ilimuradi yeye anafaidika kwa njia moja ama nyingine.

Katiba na sheria nzuri zinaweza kupunguza ama kumfanya kiongozi mwenye tabia mbaya kuacha kabisa ama kupunguza ubaya wake kwa watu anaowaongoza, hata hivyo, hii pia itategemea kama anaiheshimu au kinyume chake.

Ushahidi wa baadhi ya nchi kuwa na Katiba nzuri katika Afrika upo, lakini katika nchi hizo hizo, wizi wa mali za umma, rushwa na kukandamizwa kwa haki za binadamu ni dhahiri.

Ni vyema kuwa na Katiba bora na sheria zinazofaa, na kama zinavunjwa, historia hujenga uhalali wa kuwarejea wanaoivunja hata kama watakuwa nje ya madaraka.

Mwandishi ashitaki DCI, DPP

Na Mloka SULUHU

MIAKA sita iliyopita, Tanzania ililigubikwa na utawala ulioendesha nchi kwa matakwa ya mtu mmoja; sheria hazikufuatwa na Katiba ilisiginwa kwa kiasi kikubwa.

Wakati huo, kiongozi wa nchi, Rais John Magufuli ndiye alikuwa serikali, nchi na taifa. Hakujali haki za binadamu na haki nyingi ziliporwa kutoka kwa watu wengi.

Woga ulitawala wakati huo na hakuna aliyethubutu kumkemea, huku taasisi za haki na vyombo vya usalama vikishindwa kutofautiana naye, kwani vilishiriki kuvuruga haki.

Hata hivyo, baada ya Magufuli kufariki dunia – Machi 17, 2021, na Tanzania kuongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, uonevu ambao ulikuwa unafunikwa na kila taasisi na ofisi za serikali, sasa unanza kuhojiwa na pengine kutafuta “amani” kwenye vyombo vya sheria.

Ni kutokana na msingi huo, mwandishi wa habari na mwanaharakati nchini Tanzania, Luqman Maloto anataka mahakama itamke kwamba baadhi ya ofisi na serikali zilishindwa kufanya kazi zake kwa mujibu wa katiba na kunyamaza badala ya kuchukua hatua kukomesha ama kuzuia “uhalifu” unaoaminika kuagizwa na “wakubwa.”

Maloto amefungua kesi Mahakama Kuu Dar es Salaam akitaka itamke kuwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) na Mkurugenzi Mkuu wa Mashitaka (DPP), zilishindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati huo.

Kwamba anaiomba mahakama hiyo itamke kuwa ofisi hizo za watendaji na wasimamizi wa haki zimeshindwa kuwajibika ipasavyo katika kufuatilia na kuusaka ukweli kuhusu kushambuliwa kwa risasi kwa Makamu wa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu.

Lissu alishambuliwa kwa kumiminiwa



Tundu Lissu.

risasi na kile kinachoelewa na serikali kuwa ni “watu wasiojulikanma,” akiwa anatoka kwenye kikao cha Bunge jijini Dodoma Septemba 7, mwaka 2017.

Maloto pia anataka mahakama hiyo itamke kwamba ofisi hizo za serikali zimeshindwa kufanya majukumu yake kwa kutoeleza umma nini hasa kilitokea hadi kutekwa, kupotea na kutoonekana hadi leo kwa mwandishi wa gazeti la Mwananchi, Azory Gwanda.

Gwanda alitoweka katika mazingira ya kutatanisha akiwa nyumbani kwake Kibiti, Pwani Novemba 21, 2017 ambapo inadaiwa alitekwa na “watu wasiojulikana” na hadi leo hajulikani alipo.

Maloto anaiomba mahakama hiyo pia itamke kuwa ofisi hizo zimeshindwa kutekeleza majukumu yake na kuueleza umma nini hasa kilitokea kwa Ben Saanane, aliyekuwa msaidizi wa Freeman Mbowe.

Ben Saanane alitoweka katika mazingira ya kutatanisha kuanzia Novemba 14, 2016 na inadaiwa kuwa alitekwa na walewale – “watu wasiojulikana” na hadi leo hajulikani alipo.

Pia watu wengine wengi wanatajwa kwenye orodha hiyo.

Kupitia uwakilishi wa Wakili Hekima Mwasipu wa taasisi ya Matwiga Law Chamber, kesi hiyo iliyosajiliwa kwa namba 5 ya mwaka 2023, imepangwa kuanza kusikilizwa Februari 8 mwaka huu na kwamba itakuwa mbele ya Jaji John Nkwabi.

Wanunuzi parachichi kupewa vibali**Na Scovya MANASE**

UMASIKINI wa wakulima umekuwa ukielezwa kuchangiwa kwa kiasi kikubwa, ukiacha mambo mengine – na madalali ambao “huwalalia” bei.

Kila msimu wa mavuno unapofika – katika maeneo mengi ya Tanzania, madalali huonekana wakiwashawishi wakulima kuuza mazao yao na kuwapa bei ya chini, huku wao – baadaye kuuza kwa bei ya juu kwa wafanyabiashara.

Madalali hawa wamekuwepo pia Njombe ambapo “huwaingiza mjini” wakulima wa viazi mvingo na sasa wanahamia kwa wakulima wa parachichi.

Ili kukomesha unyonyaji huo wa wakulima, Halmashauri ya Mji wa Njombe imeanza kutoa vibali kwa wanunuzi makini wa zao hilo ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata bei nzuri ya parachichi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Njombe, Kuruthum Sadick jana aliitisha kikao kikubwa kwa wadau wa zao hilo ambalo sasa linaongoza kwa kuongeza mapato ya wakulima Njombe kwa lengo la kuwapa vibali wanunuzi wa zao hilo. Lengo la vibali hivyo ni kudhibiti madalali na kuhakikisha kuwa wanunuzi makini tu, ndiyo wanahusika katika biashara ya parachichi.

Katika hatua nyingine ya kudhibiti madalali, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka amepiga marufuku kuwepo kwa madalali.

Mkuu huyo wa mkoa anaeleza kuwa ni marufuku kwa madalali kuonekana mashambani wakiwashawishi wakulima kuuza mazao yao kwa bei ya chini.

Mtaka anasema kuwa kuanzia sasa hataki kuwaona madalali wakiingia mashambani kulangua parachichi na badala yake wakulima wauze wenyewe kwa wafanyabiashara kwa bei nzuri watakayokubaliana.

“Mkulima akipata bei nzuri ndiyo mwanzo wa kuwa na maisha bora, na bei hiyo anaipata kutoka kwa wanunuzi



Mkurugenzi Halmashauri ya Njombe, Kuruthum Sadick

makini, lakini siyo madalali ambao wao lengo lao ni kumlalia mkulima ili wauze kwa bei ya juu zaidi,” anaeleza mkuu huyo wa mkoa.

Anasema kuwepo kwa kampuni zinazonunua parachichi mkoani kwake ni hatua nzuri kwa wakulima kujihakikisha bei nzuri itakayowaondoa kwenye umasikini haraka.

Wiki iliyopita wakati akifungua Ofisi za Kampuni ya Avo Africa, wanunuzi wakubwa wa parachichi nchini, Mtaka aliwashauri kuhakikisha wanawapa bei nzuri wakulima na siyo “kuwanyonya.”

Mkurugenzi wa Kampuni ya Avo Afrika, Nagib Karmal amesema kuwa watahakikisha wananunua parachichi zote aina ya Weso na Hasi na malipo kulipa wakulima haraka. Aina hizo za parachichi ndiyo zenye soko kubwa nje ya nchi.

Pambazuko limeshuhudia kuwepo kwa ongezeko kubwa la madalali katika kipindi hiki mjini Njombe kwa kuwa ndiyo kipindi cha mavuno ya parachichi na mazao mengine, ikiwamo viazi mvingo.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika ameiomba serikali kuhakikisha walanguzi wa parachichi na mazao mengine, wanazuiwa kurubuni wakulima kuuza kwa bei ndogo – kwani kufanya hivyo ni kuongeza umasikini kwa wananchi.

Rais Ruto aomba msamaha

**Na Mwandishi WETU,
Nairobi**

KUOMBA msamaha ni kitendo cha kiungwana na kamwe siyo woga wala kujidhalilisha.

Ujasiri huu ndiyo aliofanya Rais wa Jamhuri ya Kenya, Dkt. William Ruto juzi – Jumamosi alipomualika wakili msomi na mwanaharakati wa haki za binadamu nchini humo, Dkt. Miguna Miguna na kueleza namna alivyokuwa “akisikitishwa na uonevu dhidi yake.”

Rais Ruto alimuomba msamaha kwa kile kinachoelezwa kuwa ni “ukatili” mkubwa aliofanyiwa na serikali iliyoipita, ikiongozwa na Uhuru Kenyatta.

Kupitia akaunti yake ya Twitter, Dkt. Miguna anasema kuwa alikubali msamaha huo na kwamba amesamehe yote yaliyofanywa dhidi yake na Wakenya wengine.

“Rais William Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya na Amiri Jeshi Mkuu, mapema leo ameniomba msamaha kwa niaba yake na niaba ya serikali kwa unyama niliofanyiwa na serikali iliyoondoka. Ninakubali ombi lake la msamaha,” Miguna amesema.

Dkt. Miguna anasema kuwa amekubali msamaha huo kwa kuwa umetolewa na kiongozi muungwana ambaye ameona makosa yaliyofanyika dhidi yake. Wakati wa uongozi wa Kenyatta, Ruto alikuwa Makamu wa Rais.

Anasema kuwa kilichofanywa na Serikali ya Uhuru Kenyatta ilikuwa kinyume na Katiba ya Kenya na misingi ya sheria na ubinadamu.

Kufuatia hatua hiyo ya Rais Ruto kuomba msamaha, aliyekuwa kamishna wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), Roselyn Akombe amesema kuwa ombi hilo “lilichelewa sana” na kuongeza kuwa hakuna Mkenya anayestahili kupitia yake aliyopita Miguna.

“Ombi la msamaha limechelewa sana, lakini ni vyema kwamba limefanyika sasa, hakika hakuna binadamu anayestahili



Rais Ruto akisalimiana na Miguna alipomkaribisha Ikuu, Nairobi kwa mazungumzo Jumamosi iliyoipita.

kupitia machungu yote ambayo Daktari Miguna Miguna alipitia,” amesema Akombe.

Dkt. Miguna, alitimuliwa nchini Kenya kwa madai kwamba siyo raia wa nchi hiyo Machi, 2018 baada ya “kukwaruzana” na serikali aliyokuwa akiiongoza Rais Kenyatta.

Januari 3-, 2018, Miguna alihusika kumwapisha Raila Odinga kuwa “Rais wa Umma” - kwamba ndiye alishinda uchaguzi wa Kenya uliofanyika Oktoba 2017. Kenyatta ndiye alitangazwa na Tume ya Uchaguzi na baadaye Mahakama ya Juu kwamba ndiye mshindi.

Mwezi Machi 2018, Miguna alitimuliwa nchini kwa lazima na kuziwa kurejea baada ya Serikali ya Kenyatta kumwekea vikwazo vya kusafiri – na kunyang;anya pasipoti.

Dk. Miguna alirejea Nairobi mwishoni mwa mwaka jana na amekuwa akimuunga mkono Rais Ruto kwa maelezo kwamba ndiye kiongozi bora kupata kutokea Kenya.

Katika harakati za uchaguzi mkuu wa Kenya, Miguna alikuwa akimfanyia kampeni Ruto kupitia mitandao ya kijamii, huku akimtaja kuwa ndiye kiongozi anayefaa kwa sasa kuongoza taifa hili. Alikuwa mpinzani mkubwa wa Raila huku akimuita kuwa ni “tapeli.”

Namna ya kufikia rasilimali

Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA

KAWAIDA wale wanaopambana (kama wanaharakati) ili kuleta mabadiliko katika jamii hufanya hivyo kwa sababu wameona kwamba watawala na wanasiasa kwa jumla hawatilii maanani juhudi za kufanya maisha ya watu kuwa bora.

Hufanya hivyo kwa uelewa kwamba mchakato wa kuboresha maisha ya jamii hutegemea sana mgawanyo wa nguvu na kwamba nguvu nyingi ziko wapi katika jamii. Jambo la mgawanyo wa nguvu tulilizungumzia katika makala za nyuma.

Suala la kuboresha maisha ya jamii hutegemeana sana na sera na sheria zilizopo. Ikiwa nguvu nyingi ziko mikononi mwa wasiopenda maboresho au wenye ubinafsi, basi kwa hakika zitatungwa sera na sheria legelege zinazolinda maslahi yao tu.

Pamoja na kuhitajika nia njema ya kisiasa katika kufanya maboresho ya haki za jamii, ni lazima pia kuwa na watendaji waliotaalumika vizuri na walio makini katika kuandika sera na sheria hizo na pia wasimamizi wazuri wa utekelezwaji wake.

Hawa ndio injini inayoendesha shughuli za siku kwa siku katika kuihudumia jamii. Wakati wanaharakati na wanasiasa wanapiga kelele huko nje, wataalamu watawala hawa hujifungia ndani wakifanya kazi ya kugeuza kelele hizo kuwa sera na sheria bora za kuleta mabadiliko chanya.

Katika kufanya kazi hiyo, zipo kanuni za misingi ya kuzingatia ili kudhihirisha ugawaji ubora wa haki za jamii. Hapa nitajadili moja kati ya kanuni hizo ambayo ni ufikiaji wa rasilimali na huduma za muhimu.

Uwepo wa fursa sawa katika ufikiaji wa rasilimali na huduma muhimu ni changamoto kubwa katika jamii nyingi duniani. Mjadala juu ya kanuni hii una sura nyingi kwa sababu ni dhahiri



Rais Samia. Msimamizi mkuu wa haki Tanzania kwamba kama inavyosomeka, inafikiwa kwa kushinda vikwazo vingi. Kanuni hii hakika inabeba uzito mkubwa katika kupima haki ya jamii.

Nilizungumza awali kwamba kila jamii ina vigezo vyake vinavyoongoza katika namna ya kugawa rasilimali na kutoa huduma kwa jamii. Vilevile jinsi ya kugawa kipato na utoaji wa huduma muhimu.

Tunaona wazi katika vyombo vya habari sehemu mbalimbali duniani ambako hutokea maandamano watu wakidai ama nyongeza za mishahara na stahiki nyingine.

Mambo kama hayo yanaonyesha wazi makundi fulani ya watu katika jamii kutoridhishwa na utoaji haki fulani katika jamii.

Katika mazingira yetu tulipita nyakati ngumu za mamlaka za serikali kukandamiza haki za watu kama vile watu “kutumbuliwa” pasipo kufuata sheria na taratibu.

Tuliona pia wafanyakazi kutopandishwa vyeo/madaraja na kutopandishwa mishahara. Tulisikia vilio vya wafanyabiashara kuporwa mali zao na mambo mengine ya hovyo yaliyokuwa yakikiuka misingi ya utu na Katiba.



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Pongezi, angalizo kwa Masoro

NIANZE makala kwa samahani kwa safu hii kutokuwepo katika toleo lililopita. Hii ilitokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wangu.

Januari 3 mwaka huu, Rais Samia Suluhu alimteua Ndugu Said Masoro kuwa Mkurugenzi Mkuu mpya wa Idara ya Usalama wa Taifa. Ndugu Masoro aliteuliwa kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na mtangulizi wake, Kamishna Diwani Athumani, aliyeteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Ikulu, kabla ya uteuzi huo kutenguliwa na Rais Samia.

Safu hii inampongeza Ndugu Masoro kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo muhimu.

Ndugu Masoro amekabidhiwa jukumu hilo katika kipindi mwafaka, kwani hivi karibuni tu, Rais Samia alianzisha mchakato wa kufanya mageuzi katika utendaji wa vyombo vya ulinzi na usalama, ambapo aliteua wajumbe wa sekretarieti na kamati kuhusu ajenda hiyo.

Kwahiyo, inatarajiwa kuwa Ndugu Masoro atamsaidia Rais Samia katika azma yake hiyo yenye maslahi makubwa kwa taifa.

Kama “veterani” wa Idara ya Usalama wa Taifa, ni wazi kuwa Ndugu Masoro anafahamu changamoto mbalimbali zinazoikabili taasisi hiyo nyeti.

Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na taswira iliyojengeka “mtaani” kwamba taasisi hiyo inaendeshwa kisiasa, ambapo mara kadhaa imekuwa ikituhumiwa kukisaidia chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika mambo mengi na kuwakandamiza wapinzani.

Vilevile kuna changamoto kuhusu mfumo wa ajira za taasisi hiyo ambapo “kama ilivyo kwenye taasisi nyingine muhimu,” inadaiwa kuwa ajira zimekuwa zikitolewa kwa misingi ya kufahamiana.



Said Masoro

Kadhalika, kumekuwa na malalamiko ya wananchi wengi tu kupewa vitisho na baadhi ya maafisa wa Idara ya Usalama wa Taifa. Katika hili, majuzi tu nilikuwa mhanga baada ya kuchapisha makala katika blogu yangu iliyohusu mabadiliko ya uongozi kwenye taasisi hiyo, pamoja na kutaja fursa na changamoto kwa Ndugu Masoro. Nilitumiwa vitisho kadhaa.

Pia kuna changamoto ya ugaidi wa kimataifa. Katika tathmini ya mwaka huu 2023, inatarajiwa kuwa kundi la kigaidi la Islamic State litazidisha jitihada zake kujitana barani Afrika na huenda likaelekeza nguvu zake nyingi Afrika Mashariki kutokana na sababu kadhaa.

Hata hivyo, habari njema kwa Ndugu Masoro ni ukweli kwamba changamoto zinaweza kugeuzwa kuwa fursa. Ni matumaini kwamba badala ya kutafsiri ukosoaji wenye lengo la kujenga (constructive criticism) kuwa kama “uhaini”, kiongozi huyo atasikiliza na kufanyia kazi yale atakayoona yana tija na kutoa umuzi wa haki kwa neema ya Tanzania na watu wake.

Mwisho, safu hii inatamtakia kila la heri Ndugu Masoro katika majukumu yake katika wadhifa huo mpya.

Manusura wa Precision kulipwa Sh. milioni 70

Na Mwandishi WETU

MANUSURA 19 katika ajali ya ndege ya Precision Air iliyotokea Novemba 6, mwaka jana – nje kidogo ya Uwanja wa Ndege wa Bukoba, wataambulia malipo ya fidia ya Sh. milioni 70.2, Pambazuko linaweza kueleza.

Taarifa za awali ambazo Pambazuko limepokezwa wakati likienda mitamboni jana usiku, ni kwamba fedha hizo zitakatwa kiasi cha Sh. milioni 11.7 ambazo kila mmoja aliyenusurika katika ajali hiyo alilipwa wiki iliyopita, ikielezwa kuwa ni malipo ya awali kusaidia mahitaji ya tiba na kujikimu.

Endapo kiasi hicho kitakatwa kutoka kwa waguswa hao, kila mmoja atabaki na Sh. milioni 58.5.

Kutokana na mchanganuo ambao Pambazuko limeuona kwa haraka ni kwamba kampuni zilizopewa kandarasi ya kulipa fidia hizo, zitatoa takribani Sh. bilioni 1.34, ikiwa gharama ya kubadili fedha itakuwa dola moja ya Marekani kwa Sh. 2,340.

Hata hivyo, haikufahamika mara moja endapo haya sasa ndiyo malipo ya mwisho au vinginevyo na haikujulikana lini wataanza kulipwa fedha hizo za fidia.

Pambazuko limefuatilia kwa uongozi wa juu wa Precision Air ambao watendaji wote walikataa kuzungumza kuhusu malipo haya.

Hata hivyo, mmoja wa wakurugenzi wa bodi alizungumza kwa masharti ya kutoandikwa gazeti alikiri kufikiwa kwa hatua za mwisho-mwisho ili “kumalizana na manusura hao.”

“Labda nikudokeze tu kwamba mchakato wa kuwalipa unafanyika kwa umakini mkubwa na kwamba watalipwa

haraka, ingawa sijui kiasi watakacholipwa kwa awamu inayofuata.”

Mwenyekiti wa Chama cha Kampuni za Bima Tanzania, Khamis Suleiman amesema kuwa inapotokea ajali ya ndege bima inatakiwa kumlipa aliyekumbwa na ajali hiyo kiasi cha fedha kisichopungua Sh. milioni 300.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo ya ndege iliyopata ajali, Patrick Mwanri amekuwa akisisitiza kuwa malipo ya manusura hayo yatafanyika kwa usiri mkubwa.

Kamishna wa Bima nchini Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware amesema kampuni ya Precision Air itafidiwa zaidi ya Sh. bilioni 116 kwa hasara ya kupoteza ndege yake huku akieleza manusura na wale waliopoteza maisha kufidiwa kiasi kinachoweza kufikia Sh. milioni 396.

Ndege sampuli ya ATR 42-500 hutengenezwa na kampuni ya ATR Aircraft ya Ufaransa. Sampuli hii imekuwa ikitengenezwa kati ya mwaka 1944 hadi mwaka 2012. Inahitaji marubani wawili na inaweza kubeba abiria 42. Huweza kuruka hadi futi 25,000 kwenda juu angani na kasi yake hufikia maili 345 kwa saa. Bei yake ni wastani Sh. bilioni 28.34.

Manusura hao 19 ni miongozi mwa abiria 43 walioelezwa kuwamo ndani ya ndege aina ya ATR42-500 mali ya Shirika la Precision iliyolazimika kutua Ziwa Victoria, mita 150 kutoka Uwanja wa Ndege wa Bukoba.

Ndege hiyo yenye usajili 5H-PWF namba PW 494 iliyoanza safari yake kuelekea Bukoba alfajiri ya Jumapili, Novemba 6, mwaka huu, iliingia anga la mji huo pembezoni mwa Ziwa Victoria, lakini rubani wake, Buruani Rubaga alishindwa kutua uwanjani kutokana na hali ya hewa kuwa mbaya.

Samia akarabati mwavuli wa siasa



Rais Samia

Na Mwandishi WETU

SIFA mojawapo ya nchi inayoendeshwa kwa kuzingatia misingi ya demokrasia ya uwakilishi ni kuwepo kwa uhuru wa kuunda vikundi, vikiwamo vyama vya siasa na azaki kukusanyika ndani na hadharani bila vikwazo holela, ilimradi hakuna sheria inayevunjwa.

Katika sekta ya kisiasa, uhuru wa kuunda vikundi – ikiwa ni vyama vya siasa kukusanyika hadharani bila vikwazo holela ni fursa muhimu kwa ajili ya kuviwezesha vyama vya siasa kutafuta wanachama wapya na kutekeleza jukumu lake la kukosoa utendaji kazi wa serikali inayoongozwa na chama tawala.

Umantiki wa jukumu lake la kukosoa utendaji kazi wa serikali inayoongozwa na chama tawala iliwahi kuelezea vyema na Padre Bernard Joinet, katika miaka ya 1980, kupitia andiko lake litwalo “A letter to my superiors: On multi-party democracy.” (Barua kwa wakubwa zangu kuhusu demokrasia ya vyama vingi).

Katika barua hii, Joinet anasema kuwa, demokrasia ni kama mwavuli wa kujikinga na jua na mvua. Kwa kawaida,

mwavuli unazo sehemu tatu. Kuna nguo yenye umbo la duara, ambayo hukunjwa na kukunjuliwa kila inapobidi; njiti (spokes) za kukunjua kitanbaa cha mwavuli; nguzo inayounganisha kitambaa na njiti; na kitasa cha mwavuli kinachotumika kufyatua na kufyata njiti.

Mwavuli mzuri ni ule unaofanya kazi inayopaswa kufanywa na mwavuli. Yaani kumkinga mtu dhidi ya miale ya jua na matone ya mvua.

Kusudi kazi hiyo ifanyike vizuri ni lazima njiti zote za mwavuli ziwe zinafanya kazi sawasawa na kwa wakati mmoja. Ikitokea njiti mojawapo ikavunjika, mwavuli hautafanya kazi yake ipasavyo.

Hali iko hivyo katika ulimwengu wa demokrasia ya vyama vingi. Mduara wa kazi ya kujenga nchi, huanzia kwenye kampeni za uchaguzi, ambapo kila chama cha siasa huunda ilani yake na kuinadi kwa wapigakura.

Chama kinachoshinda uchaguzi kwa kura nyingi huunda serikali na kuanza kutekeleza sera zilizomo kwenye ilani yake ya uchaguzi.

Samia akarabati mwavuli wa siasa*Inatoka Uk. 11*

Utekelezaji wa sera za serikali hufuatiwa na vyama vya siasa vilivyoko katika kambi ya upinzani. Vyama hufanya kazi hii kupitia ndani ya Bunge na pia kupitia nje ya Bunge kwa njia ya mikutano ya hadhara.

Awamu moja ya utekelezaji wa ilani ya chama tawala inapokamilika, hufuata awamu nyingine ya uchaguzi, ambapo ilani mpya huandaliwa na kunadiwa, na hivyo mduara wa ujasiriadola kuanza tena.

Kwa sababu hii, kama baadhi ya vyama vya siasa havina fursa ya kufanya mikutano ya hadhara, kazi ya kukosoa utendaji kazi wa serikali haitafanyika.

Na hii maana yake ni kwamba, baadhi ya njiti katika mwavuli wa demokrasia ya vyama vingi zimeteguka kiasi cha kutofanya kazi yake ipasavyo.

Kwa mantiki hiyo, hata mfumo wa demokrasia unakuwa umepoteza sifa ya kuitwa mfumo mzuri wa kidemokrasia. Yaani, mwavuli wa kidemokrasia unakuwa umepoteza uwezo wa kuwakinga wananchi dhidi ya miale ya jua ya uzembe serikalini, kama ambavyo unakuwa umeshindwa kuwalinda dhidi ya matone ya mvua ya ukandamizaji kutoka serikalini.

Mara nyingi, pasipo fursa ya vyama vya upinzani kukutana na umma mpana, uzembe na ukandamizaji hushamiri ndani ya serikali.

Hivyo, uamuzi wa Rais Samia wa kuondoa zuio la mikutano ya hadhara kwa vyama vya upinzani ni uamuzi wenye tija kwa nchi.

Akiongelea uamuzi wa Rais Samia, Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Dodoma, Adam Kimbisa, alieleza vyema mawazo haya.

“Bila mikutano vyama vya upinzani havina fursa ya kuishitaki serikali kwa wananchi wala kupata wanachama wapya. Hata sisi watu wa chama tawala, tutabweteka kiasi cha kupuuzia kwenda

**Freema Mbowe, kiongozi wa upinzani**

kwa wananchi kuwapa mrejesho wa nini kinafanywa na serikali,” alisema Kimbisa.

Kwa sababu hii, Mwalimu Adolfo Mwakitalima wa Mbeya Mjini aliliambia Pambazuko kwamba, sasa ni wakati wa vyama vya upinzani kuwatetea wananchi kazi waliyoshindwa kufanya kwa miaka saba.

“Tangu Rais Magufuli alipoppingia madarakani, vyama vya upinzani vilipigwa pini (viliwekewa zuio). Wakati huo Rais Samia alikuwa Makamu wa Rais. Sasa Samia ni rais na ameruhusu mikutani ya hadhara...

... Wapinzani washindwe wenyewe kwa sababu za kiuchumi, maana kuna msema kwamba ‘adui mwombe njaa’ unasikika sana huku mitaani,” alisema Mwakitalima.

Kwa kutumia mfano wa mwavuli, tunaweza kusema kwamba, Rais Samia amekarabati mwavuli wa demokrasia ya vyama vingi hapa nchini Tanzania, kiasi cha kujiongeza fursa ya ushindi katika uchaguzi ujao.

Kuhusu jambo hili, Mhandisi Rudolf Kamaleki wa Morogoro mjini aliliambia Pambazuko kwamba “Rais Samia ameona mbali kuliko watu wanavyoweza kufukiri, maana sasa amekwishapangua swali moja ambalo angeulizwa jukwaani mwaka 2025, kuhusu sababu za kukataza mikutano ya hadhara ya wapinzani.”

Yuko wapi Dkt Mashali wetu?

Na Mwandishi WETU

WAPO watu duniani wenye ‘utukufu’ ambao unaweza kuelezwa na kila mmoja na wala usisubiri kupitishwa na kundi la watu kutokana na mchango wao kwa binadamu.

Hawa ni wachache, lakini wapo na kwamba njia zao njema hazipazwi na vyombo vya habari wala kuwatumia waandishi kueleza mchango wao wenye kutukuka.

Mmoja wa watu hao ni daktari wa Misri, Muhammad Mashali. Huyu ni mzaliwa wa nchi hiyo na alifanya kazi katika eneo moja linaloitwa Tanta.

Sifa yake kubwa inatokana na tabia yake ya kujitolea kuhudumia wagonjwa masikini kwa kuwatibu biure kwa zaidi ya miaka 50.

Wakati anaendelea na masomo ya juu ya udaktari, Muhammad aliapa kwamba kamwe hatachukua pesa ya wagonjwa masikini kuwatibu.

“Niliapa kwa Mungu kwamba nisingechukua hata senti moja kutoka kwa masikini kuwatibu na kwamba ningebaki katika kliniki yangu ili kuwasaidia wapone na waendele na maisha yao,” kauli hii aliitoa Muhammad miaka 50 iliyopita na ameishi nayo miaka yote hadi alipofariki dunia mwaka 2020 – akiwa na miaka 76.

Siku ya mazishi yake, maelfu ya watu walijitokeza kutoa heshima zao na kumuaga Mashali - anayejulikana kwa urahisi kama “daktari wa masikini” - katika kijiji chake cha Zahr El-Temseh, katika Mkoa wa Beheira, kaskazini mwa Misri.

Mwili wake ulipelekwa huko kutoka mji wa Tanta, ambako aliishi na kufanya kazi.

Umati wa watu walioandamana katika msafara wa mazishi yake ulionyesha upendo, pongezi na shukrani kwa Mashali.

Daktari huyo alipata umaarufu nchini mwake kwa kazi za kutibu wagonjwa



Dkt. Mashali

bila kuwadai fedha, hasa masikini na kwa kufanya hivyo, baadhi ya ndugu wa wagonjwa wenye uwezo walimchangia vifaatiba na hata dawa ili aweze kugawa bure.

Alionyesha katika vipindi kadhaa ya televisheni na ripoti za habari, na taasisi nyingi za serikali zilimheshimu kwa kazi yake na ukarimu wake.

Daktari huyo pia aliwahi kukataa michango ya fedha kutoka kwa watazamaji wakati akihojiwa na kituo kimoja cha televisheni.

Akizungumzia uamuzi wake wa kukataa mchango wa mamilioni kutoka kwenye kipindi cha televisheni, alisema; “ninakataa michango na ninawashauri watoe michango hiyo kwa maskini na wahitaji zaidi” aliongeza.

Mashali alikulia katika familia masikini na alianza kazi yake bila kuwa na vifaatiba, maabara wala wasaidizi, lakini alitumia pesa zake kidogo alizopata wakati akifanya kazi serikalini ili kujenga kliniki ya kusaidia wagonjwa, hasa wasiokuwa na uwezo.

Inaelezwa kuwa watoto watatu wa Muhammad ni wahandisi, hivyo nafasi ya kuendeleza kliniki ya baba yao ni finyu.

Yuko wapi Mashali wa Tanzania?

Waafrika nani ametulaani?

Na Padre Titus AMIGU

RAIA wasiokuwa na maarifa yoyote; wenye ujinga wa mambo mengi na hata mazingira yao; wenye njaa na wale wenye magonjwa ni mzigo kwa nani?

Je, huo siyo mzigo wa serikali kwa hawa wote, maana ni wananchi wake na tena huenda wako katika hali hiyo kutokana na matakwa ya serikali yenyewe? Kwamba wanafanywa wajinga ili yenyewe iendelee kuongoza?

Fikiria, raia wako wanaamini kwamba wamelaaniwa, je, watajamini saa ngapi hata kuyachukua maisha yao mikononi mwao? Wao ni mzigo kuliko mifugo!

Fikiria, raia wako wanaamini ardhi za nchi zao zimelaaniwa, watajifunza saa ngapi namna ya kutumia rasilimali zao? Watajifunza lini kilimo cha kisasa?

Fikiria, raia wako wanaamini wanakumbwa na maradhi kwa sababu ardhi walipojenga nyumba zao ina mapooza, watajifunza saa ngapi kanuni za afya na lishe bora?

Fikiria, raia wako wanaamini watapata mazao mengi wakinyunyizia mashamba yao maji ya upako, watajifunza saa ngapi kilimo cha umwagiliaji?

Fikiria, raia wako wanaamini watapata mali wakinywa maji aliyooga mchungaji, watajifunza saa ngapi kutumia nguvu zao katika kilimo na ujasiriamali?

Fikiria, raia wako wanaamini watapata pesa wakivaa chupi za upako au wakila keki za upako, watajifunza saa ngapi kutumia nguvu zao katika kilimo na ujasiriamali? Watajifunza lini stadi za mikono?

Fikiria, mabinti zako wanaamini wataolewa na mabwana watakaoletwa na upepo wa kisulisuli, watajifunza lini tabia njema za kufaa kuwa wake za watu na mama wa watoto wao?

Fikiria, vijana wako wenye nguvu wanaamini watapata nyumba kwa kukesha kwenye makongamano, watajifunza lini kufyatua matofali ya kuchoma na kujijengea nyumba zao?



Sehemu ya ramani ya bara la Afrika

Fikiria, raia wako wanaamini wakijambiwa “ushuzi” na mchungaji watapata ajira, watajifunza lini kujajiri wenyewe?

Fikiria, raia wako wanaamini kwamba watapata magari wakifanyiwa maombi, watajifunza lini sayansi na teknolojia wajiundie vyombo vyoa wenyewe?

Fikiria, raia wako wanaamini kwamba wataenda Marekani na Ulaya wakifanyiwa maombi, watajifunza wapi uzalendo wa kuzijenga nchi zao wenyewe? Siyo hao watakaokubali kuwa mbwa Ulaya au Marekani kuliko kuwa watu nchini na barani mwao?

Ukijumlisha haya yote, tunashangaa nchi za Kiafrika zikiendelea kujiburuza katika umaskini wa kunuka, njaa na maradhi?

Tunashangaa nini sisi Waafrika tukiwa watembeza bakuli tu? Tunashangaa nini tunapodharauliwa na watu wa mabara mengine?

Ukijumlisha haya yote, tunashangaa nini sisi Waafrika tukipewa misaada ya aibu; ya fedha, ya mitumba hata ya chupi na sidiria?

Sisi hatuna ujanja mwingine isipokuwa kutumia mitumba ya kila sampuli: vyombo vya usafiri, nguu, vyombo vya majumbani na vingine vingi.

Sisi ni watumiaji wa vitu vilivyowahi kutumiwa. Sisi ni wauzaji wa vilivyowahi kuuuzwa. Sisi ni wanunuzi wa vilivyowahi kununuliwa. Aibu sana! Sisi tumezoa vya kunyonga, vya kuchinja hatuwezi!

Pambazuko

**Gazeti la Pambazuko sasa
kupokea matangazo**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi kwa

kuwasiliana kupitia namba hii:
0744 768 263 au Barua- Pepe;
info@pambazuko.tz

*Karibu sana Pambazuko isaidie
kupaisha na kupambazua
huduma na biashara yako.*

Ulaghai wa manabii utakoma lini?

Na Mwandishi MAALUM

IMEKUWA jambo la kawaida katika Tanzania kusikia kila uchao kuna “manabii” wameibuka. Kwamba wanaombea watu wanapona, wanapata watoto na wengine kuwa matajiri.

Kunapotangazwa kuwepo mikutano ya manabii, watu hufurika kwa ajili ya kwenda kupata “miujiza” yao, bila aibu, wanadai kuwa na nguvu za ziada kutoka kwa “mungu.”

Kimsingi, watu hawa – wengi wakiwa ni wanaume, ingawa na wanawake wameanza kuongezeka, wamejitengezea ajira ambayo uwaingizia kiasi kikubwa cha fedha kwa ulaghai wao.

Hawa wanachukua sadaka kutoka kwa kila mmoja, wakiwamo masikini wanaokwenda kujaribu kupata miujiza kutokana na maombi yao.

Manabii hawa huweka pesa mifukoni mwao kwa kuwauzia watu kile wanachodai kuwa ni “neni la Mungu.” Hawa wamejenga kusanyiko la utajiri kutoka kwa masikini. Wanatajirisha binafsi.

Ushahidi upo tele kabisa. Wengine wanajenga maghorofa. Wengine wananunua ndege. Wengine wanatembelea magari ya kifahari. Wengine wanajenga hoteli za kisasa. Wengine wanasomesha watoto wao kwenye shule bora, tena nje ya nchi kwa sadaka za masikini.

Jitafti sana wewe “uliyechangia huduma” hizi au zile za manabii hawa umebakia wapi? Siyo hoehae bado? Huna maradhi bado? Huna ufukara bado? Ukiwete umekutoka? Upofu umekutoka? Uziwi umekutoka? Ada za watoto wako

unazimudu sasa? Nyumba yako si ile ile? Mavazi yako si masurupwete yale yale? Chakula chako si cha kuungaunga bado?

Mtanzania mwenzangu zidi kujiuliza na fanya utafiti hata kidogo. Wangapi wamekuwa mabilionea baada ya makongamano mengi ya Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Makambako, Mbeya, Moshi, Musoma, Mtwara, Mwanza, Njombe, Sumbawanga, Songea au Tabora? Bila shaka, hakuna.

Sasa, basi, funguka macho ujue “umeliwa” pamoja na wenzako. Ukome basi! Makongamono ya Jangwani au Uwanja wa Benjamini Mkapa yametengeza mabilionea wangapi au yamewaponya wangapi?

Je, makongamano ya Unga Limited, Arusha? Je, makongamano ya Furahisha, Mwanza? Yamewafaidisha wangapi na kuwanasua kutoka kwenye ufukara wao?

Hivi lini watu watajifunza kuachana na mwenendo huu ambao unaonekana kuota mizizi sasa kuliko miaka mingi iliyopita?

Kimsingi, watu wamedanganywa na kuibiwa sana na hawa wanaojiita manabii Ushahidi wa kwamba hali ni mbaya na kwamba watu wamegota kufikiri hadi kutumaini maombi tu, upo tele. Ni jinsi viwanja na viwanja vya makongamano vinavyojaa watu. Hii maana yake hao wote wameshindwa kuwekeza katika akili na rasilimali za nchi na hata elimu haifai tena.

Ifahamike tu kwamba huko Ulaya, Marekani, Asia (Japani, China, Korea ya Kusini n.k.) hawakuendelea kwa sala na mikesha ya kila siku. Wametumia akili, nguvu, jasho na rasilimali.

Umefika wakati sasa wa kila mmoja kutumia akili, kufanya kazi kwa bidii na hapo ndipo ufukara utatoweka.

Unabii katika dunia ya leo

Na Benedict MSOFFE

KATIKA dini nyingi, hasa za kale; Uyahudi, Uislamu na Ukristo, nabii ni mtu ambaye aliaminika kuwa na nafasi ya kuwasiliana na Mungu moja kwa moja na kisha kuwasilisha ujumbe wa Mungu kwa hadhira fulani. Hadhira inaweza kuwa mtu mmoja, kikundi cha watu wachache au watu wote duniani.

Kwa mfano, katika Agano la Kale, Musa alikuwa ni Nabii aliyepokea ujumbe wa Mungu kwa mtu mmoja aitwaye Farao kuhusu uhuru wa wana wa Israel.

Na katika Agano Jipya, Nabii Yona alitumwa kwenda mji wa Ninawe kuwaonya juu ya hasira ya Mungu kama wasingetubu dhambi zao.

Hivyo, unabii ni dhana ambayo imekuwepo duniani tangu zamani. Lakini, manabii hawakuwa wafalme. Walitoka katika familia za kawaida. Waliwajibika kwa bidii na ujasiri na hata wengine kufa. Nabii hakuwa malaika au kiumbe wa ajabu kutoka dunia nyingine.

Alikuwa na asili yake katika jamii alimozaliwa, akalelewa, na kujifunza kuwa mtu. Nabii alipokea ujumbe maalum kutoka kwa Mungu. Ujumbe wake haikuwa ubunifu wala ujanja wake.

Nyuma ya ujumbe wa nabii zilikuwemo habari juu ya wakati alimoishi pamoja na hali ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na vinginevyo, katika wakati huo. Nyuma ya kilio, kelele na mbiu ya nabii kulikuwa na uhalisia uliotangazwa.

Ndani mwa ujumbe wa kinabii kulikuwa na ujumbe utokao chini hapa duniani, katika uzoefu wa maisha ya kila siku ya watu. Nabii alitabiri tu juu ya hali itakayokuwapo baadae, akiwa na ufahamu wa hali ya wakati uliopo.

Kila nabii alikuwa na sifa ya kuwa na ujuzi katika nyanja mbalimbali kuhusu hali ya kijamii inayomzunguka. Nabii hakuwa kasuku anayevumisha tu kila kinachovumishwa na upepo upitao.

Wala hakuwa kama msafirishaji wa mzigo asiyejua ndani kuna nini. Nabii alikijua kile kilichomo katika



Nabii Musa

jamii kilichosababisha ujio wa ujumbe aliopewa auifikishe. Alijua wapi kilipo kidonda ambacho ujumbe wake unaenda kukiponya.

Nabii hakuwa mtu mwenye taarifa alizotaarifiwa tu, bali mtu aliyefahamu uhusiano wa kweli kati ya taarifa na uhalisia.

Katika nyakati zetu zinazotawaliwa sana na wimbi la unabii wa kila namna, wakiwemo manabii wa kijamii, kisiasa, kiuchumi, na kiutamaduni, swali la msingi la kujiuliza ni hili; “je, bado manabii wanao umuhimu katika jamii ya leo inayowazunguka, na kama upo, wanatekeleza majukumu yao ipasavyo?”

Jawabu ni kwamba, bado manabii wana umuhimu katika jamii ya leo, na hasa wale wenye weledi wa msingi kuhusu sekta za utawala, siasa, uchumi, jamii, kielimu, tiba, mazingira na sekta baki.

Hilo ndilo somo kuu tumepata kutoka kwa waasisi wa teolojia ya ukombozi huko Amerika ya Kusini. Lakini yafaa tuwe makini na manabii wa uwongo (Mathayo 7:15).

Miaka 205 tangu kuzaliwa Marx

Na Holesime AKILI

WATU hutofautiana katika viwango vya ubunifu wao kwenye kuzalisha na kutumia mali. Hivyo, kihistoria, mali imekuwa ikikusanyika mikononi mwa watu wachache walio wajanja kuliko wenzao.

Hatimaye, pengo kati ya matajiri na maskini linapozidi kupanuka, maskini wengi hulazimika kujihusisha na tabia zinazotishia utulivu na amani katika jamii pana.

Hivyo, kihistoria, wanazuoni wanaotetea “jamii ya haki na amani” wamekuwa wakijadili chimbuko na tiba ya ugonjwa huu – wa kujishusha.


Miongoni mwa wanzazuoni hao ni Karl Marx wa Ujerumani, aliyependekeza mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii iitwayo “ujamaa na komunisti.” Marx alizaliwa mwaka 1818 huko Ujerumani na kufariki mwaka 1883.

Katika mtazamo wa Marx, ukomunisti ni mfumo wa nadharia ya kisayansi na vuguvugu la kuwashawishi watu kuona matatizo yao, kufanya hukumu stahiki, na kuchukua hatua za pamoja kivitendo ili kuleta mabadiliko wanayoyataka. Mfumo huu unajengwa na kanuni sita.

Kanuni ya kwanza, kanuni ya “udayalektika” (dialectics), inasema kwamba, mapinduzi ya kijamii huongozwa na kanuni ya mnyukanao kati ya “rai asilia” (thesis) na “rai mbadala” (antithesis) unaozalisha “rai hitimisho” (synthesis) yenye kutokana na rai hizi mbili zinazokinzana.

Kanuni ya pili, kanuni ya “umwili” (materialism), inayosema kwamba, vitu vyenye uzito na vinavyoweza kushika nafasi yenye ujazo maalum, yaani “miili,” ndio ukweli wa msingi hapa ulimwengu. Hii maana yake ni kwamba hata uwepo wa “roho” unategemea uwepo wa mwili.

Kanuni ya tatu, kanuni ya “veto ya kiuchumi,” inatamka kwamba “uthabiti wa sekta ya uchumi ndio unaamua uthabiti wa maisha katika sekta baki,” yaani “economic determinism.”



Karl Marx

Kanuni ya nne, kanuni ya mishahara midogo humaanisha faida kubwa, inasema kuwa mabepari huwanyonya waajiriwa wanaovujajasho kwa sababu, mwajiriwa huzalisha kitu chenye thamani kubwa kuliko malipo anayopewa, ambapo, baada ya mauzo ziada (surplus value) hubaki mikononi mwa mwajiri, ambaye hupata faida kubwa kuliko mzalishaji.

Jambo hili hupanua pengo kati ya tabaka la mabepari na tabaka la wavujajasho (progressive pauperization).

Na kanuni ya tano, kanuni ya unabii kuhusu anguko la ubepari, inasema kwamba, anguko la ubepari haliepukiki kwa sababu kuna siku itatokea “udikteta wa wavujajasho” ambao watafanya mapinduzi, kushika njia kuu za uchumi, na hatimaye kuunda jamii isiyo na matabaka ya kiuchumi.

Hata hivyo, japo lengo la Marx lilikuwa ni kupigania usawa wa binadamu, na hivyo kutetea heshima ya ubinadamu, alichagua mbinu ya “udikteta wa wavujajasho,” ambayo ni mbinu “haramu kimaadili,” kwani inavunja haki za binadamu walioko kwenye kambi ya mabepari.

Kosa la Marx linatokea leo kupitia mifumo ya kiima (totalitarian systems), kama vile utumwa, ukoloni, mfumodume, mfumo-kasisi, na udikteta.

Lakini, lengo halali halipaswi kuhlalisha mbinu haramu.

Matokeo yameshtua wengi

Mhariri,

MATOKEO ya mitihani ya Kidato cha Pili iliyofanyika mwaka jana, hakika yamenistua.

Naamini na wengine wengi wamekumbwa na wasiwasi kwamba huenda vijana wetu hawapewi elimu inayofaa au labda mitihani inatungwa bila kufuata yale waliyofundishwa darasani.

Inasikitisha zaidi kwamba masomo wanayopaswa kuyafanya kazi zaidi, hasa ya sayansi na hisabati ndiyo wamepata alama chache sana.

Ni wakati muafaka sasa wakuu wa serikali, na hasa wizara ya elimu kujipanga upya kuona ni namna gani wanakwama elimu yetu.

**Masolwa Kijah,
Kawe, Dar es Salaam.**

Tujenge tabia ya kusoma vitabu

Mhariri,

KUSOMA vitabu ni chanzo kikubwa, kizuri na rahisi kwa ajili ya kupata maarifa, lakini Watanzania wengi hawana tabia ya kuvisoma.

Inashangaza kwamba hata wanafunzi wa vyuo vyetu vikuu, hawana tabia hiyo na mara nyingi wanaonekana wakishika vitabu mitihani inapokaribia. Hii siyo tabia nzuri.

Ni vyema kila Mtanzania kujenga utamaduni wa kujisomea vitabu kwa ajili ya kuibua fursa mbalimbali za maendeleo na kuacha tabia ya kutumia vitabu kuwa sehemu salama ya kuhifadhia fedha kama wafanyavyo baadhi ya watu vijijini na mjini.

Inashangaza pia kwamba waandishi wa vitabu wamekuwa wakihimizwa kuendelea kuandika vitabu, lakini wasomaji wako wapi?

Zipo faida nyingi katika usomaji wa vitabu ikiwemo kutanua fikra, kujenga uelewa na kuwa na uwezo wa kuchambua na kuchanganua mambo mbalimbali na hivyo mtu yeyote anayesoma sana vitabu, atakuwa ni mwenye kujaa maarifa, mbunifu na mwenye maendeleo.

Pamoja na walimu kuanzia shule za awali kusoma vitabu kwa vijana, lakini ni muda muafaka sasa kwa vyuo

vikuu kuwa chachu ya kufanya hivyo na hata ikiwezekana kuanzisha vilabu vya kujisomea vitabu ili kujenga tabia ya kusoma.

Ni muhimu sana sasa kwa vyuo vikuu kuungana na dunia katika kuadhimisha usomaji wa vitabu ili kuibua hamasa na kujenga utamaduni wa kusoma vitabu kwani taifa lisilo na vitabu ni taifa mfu.

Kwa kuwa vitabu ndiyo nyenzo pekee inayoweza kuwasilisha maono na mawazo ya watu kutoka kizazi kimoja kwenda kingine, ni vyema kuhimiza usomaji wake kuanzia sasa.

Kitu kingine muhimu ni wananchi kujenga tabia ya kuheshimu watunzi na waandishi wa viabu, kwani hii itawaongezea hamu ya kuandika zaidi na zaidi.

Kuwaheshimu waandishi hao ni kununua na kusoma vitabu na siyo kukutana nao na kuwapa shikamoo au heshima nyingine ya kijamii.

Kuheshimu waandishi wa vitabu kutawatia moyo kuendelea kuandika zaidi hivyo kuwa na nafasi ya kusomwa tena na tena na kujihakikishia taifa lenye watu wenye utambuzi wa mambo mengi na hata weledi.

**Mwalimu Adam Malendeje,
Ngudu, Kwimba – Mwanza.**

Tunapokea Barua

Mhariri anapokea barua kutoka wasomaji wake kwa ajili ya kuzichapisha ama kuzitafutia majibu kutoka ofisi za serikali na binafsi. Tuma barua yako kwa njia ya barua-pepe: info@pambazuko.tz au kupitia namba ya simu: 0744 768 263

Matibabu asili nyumbani

Na Mwandishi MAALUM

MAISHA ya mwanadamu yamejaa changamoto nyingi, ikiwamo magonjwa ya kuambukizwa na mengine yanayotokea wa njia zingine.

Magonjwa mengi yana tiba zake; zipo za hospitali na zingine za asili, hata kama sayansi inazipinga kwa maelezo kwamba “hazijathibitishwa.”

Matunda, magome ya miti, majani na vyakula anuai, vinaelezwa kuwa vinaweza kuwa tiba ya baadhi ya magonjwa kama inavyoelezwa hapa;

Ikiwa mtu anasumbuliwa na gesi tumboni na yuko nyumbani, kwa haraka anaweza kula tango, baada ya kuliosha likiwa na maganda yake. Hapo atapata anafuu haraka na kama hali itazidi, basi anaweza kwenda hospitali.

Ikiwa kuna mtu nyumbani na anasumbuliwa na tatizo la kutopata choo, anashauriwa kunywa maziwa mtindi.

Ikiwa nyumbani kuna tu anasumbuliwa na shinikizo la juu (presha ya kupanda) anashauriwa kutafuna ndizi mbivu kwani inashusha haraka

Ikiwa kuwa mtu anaharisha, ni vyema akanywa kahawa ambayo ameweka matone kadhaa ya limao, tiba hii ya haraka inaweza kuwa msaada zaidi kwa wagonjwa wa mafua.

Endapo kuna mgonjwa anasumbuliwa na misuli kukaza, anashauriwa kula parachichi kwa sababu tunda hilo lina magnesium nyingi, hivyo ni tiba nzuri zaidi.

Kama nyumbani kuna mgonjwa ambaye anasumbuliwa na mafuta mengi kwenye mishipa ya damu (cholesterol), anashauriwa kula vipande vya bilingani iliyomenywa kabla ya kulala kwani inafanya kazi vyema zaidi.

Ikiwa kuna watu wamejaa hofu na uwoga – hasa wakati wa usiku ni vyema wakanywa chai ambayo ina majani ya



Matunda mengi ni tiba

chamomile.

Kama kuna mtu hapati usingizi wa kutosha ama unachelewa kuja, ni vyema akanywa shomari inafanya kazi kama dawa za usingizi

Mbali na matumizi ya matunda na vyakula, mwili wa binadamu unataka ushughulishwe kidogo, siyo kubweteka na kuulaza kila mara, kwani ni mwanzo wa kuleta magonjwa.

Hivyo ni vyema kufanya mazoezi mara kwa mara, ambapo mishipa itakuwa ikipata mwanya wa kupitisha vyema damu na hata kuzifanya nyama za mwili kuwa imara zaidi.

Ileweke kuwa zoezi la kutembea ni zuri zaidi kwani huipa mishipa mingi nafasi ya kufanya kazi vyema zaidi kuliko viungo vingine.

Miguu yote kwa pamoja ina asilimia 50 ya mishipa ya fahamu ya mwili wa binadamu, asilimia 50 ya mishipa ya damu na asilimia 50 ya damu inapita ndani yake, hivyo zoezi la kutembea ni bora zaidi.

Hivyo basi, mazoezi ya kutembea angalau mara mbili kwa wiki, ni muhimu sana kwa afya ya mwili na akili.

Mtihani kuyeyusha imani mgando

Na Deusedith KAHANGWA

PROFESA Saul Aron Kripke (1940-2022) wa Marekani, aliandika kitabu, “Philosophical Troubles (2011).” Katika sura ya pili, anajadili “kituko cha imani mgando,” yaani “dogmatism paradox,” na jinsi ya kuziyeyusha imani hizo.

Anatumia neno “imani” kumaanisha seti ya mawazo, fikra au kanuni zilizo kichwani mwa mtu katika wakati fulani, bila kujali kama ni imani nyoofu au imani potofu. Mifano ni imani kwamba, “vitu viwili kujumlisha vitu vitatu ni vitu vitano” na “jukumu la serikali ni kukuza na kuhami maslahi ya raia wote.”

Na anatumia maneno “imani mgando” kumaanisha imani walioendelea kukumbatiwa na watu waliobweteka kifikra kiasi cha kupuuzia ushahidi kinzani wenye kuonyesha kwamba imani yao ina upotofu fulani.

Kwa mfano, Kanuni ya Imani ya Nikea (325BK), ni imani inayojumuisha seti ya matamko muhimu 11. Lakini, seti hii inaambatana na upotofu wa kimantiki. Tatizo liko hivi:

Kwa kuwa “Mungu anazo nafsi tatu,” na kwa vile “Yesu anayo nafsi moja,” basi “Yesu siyo Mungu”; kwa kuwa “Mungu anazo nafsi tatu,” na kwa vile “Baba anayo nafsi moja,” basi “Baba siyo Mungu”; na kwa kuwa “Mungu anazo nafsi tatu,” na kwa vile “Roho Mtakatifu anayo nafsi moja,” basi “Roho Mtakatifu siyo Mungu.”

Hata hivyo, Kanuni ya Imani ya Nikea inasema kwamba, “Yesu ni Mungu,” kwamba “Baba ni Mungu,” na kwamba “Roho Mtakatifu ni Mungu.”

Hivyo, Kanuni ya Imani ya Nikea inabeba mkanganyiko wa kimantiki na kiontolojia kuhusu Mungu. Huu ni mkanganyiko wa kiteolojia.

Kuna mikanganyiko kama hii kwenye siasa, uchumi, jamii, afya, elimu, mazingira na kwingineko. Mikanganyiko



Prof. Saul Kripke

hii hujulikana kwa rai wachache wa vijijini. Lakini inajulikana kwa wanazuoni wengi wakiwemo wasiasa.

Hawa wanafahamu kwamba, mtu akikwambia jambo potofu, wakati anajua kwamba ni potofu, na anajua kwamba unajua kuwa ni jambo potofu, lakini ukalikubali kwa sababu ya kubembeleza urafiki wa Kaizari, unakuwa umedharau utu wako na yeye anakudharau kwa sababu unajidharau.

Ni kwa kutumia mantiki hii, Kripke anaibua kituko cha “imani mgando” zinazotetewa na baadhi ya wanazuoni bila kujali upotofu wake, wakiwahimiza wafuasi wao kuendelea kuzikumbatia, kwa sababu ya ushawishi unaoanzia kwenye madai kwamba, watapata majibu ya maswali yao wakifika katika ulimwengu ujao.

Hata hivyo, kuna sababu nzuri za kuyeyusha “mawazo mgando” bila kusubiri kufika katika ulimwengu ujao.

Hivyo, tupambane na utumwa wa “mawazo mgando” kwa kuhakikisha kuwa mateka na watekaji wao wanafahamu ushahidi mpya tulio nao unatamka nini; unamaanisha nini dhidi ya imani yao ya sasa, na kwa vipi ushahidi huo utumike kuboresha imani hiyo.

Kizungumukuti cha Fei Toto

Na Yusuf ABOUT

SAKATA la mchezaji wa Yanga, Feisal Salum Abdalla (Fei Toto), bado bichi na linaonekana kumuweka njiapanda, akifikiri akate rufani ama aache ili aendelee kuichezea timu yake hiyo.

Hata hivyo, huenda kwa kiasi kikubwa; roho yake haipo Yanga, ingawa mwili sasa unalazimishwa na sheria na taratibu zinazoongoza mchezo huo maarufu zaidi duniani – kuichezea timu hiyo ya Jangwani, Dar es Salaam.

Wiki iliyopita, Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) ilitoa uamuzi kwamba mchezaji huyo ni halali wa klabu hiyo kwa mujibu wa mkataba uliopo na waajiri wake, baada ya kubaini kuwa alivunja baadhi ya sheria katika nia yake ya kuondoka kwenda kujiunga na timu nyijine.

Baada ya uamuzi huo, Fei Toto anadaiwa kutamani kukata rufaa kupinga uamuzi huo, ingawa kufanya hivyo kunaonekana kuwa na hasara zaidi kwake kuliko faida anayoitegemea. Tuone baadhi ya hasara hizo.

Endapo mchezaji huyo atapeleka shitaka lake, kwenye Mahakama ya Usuluhishi (CAS) ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA) kuna uwezekano mkubwa wa kushindwa mapema kwani imedhihirika kuwa alighafirika kufikia uamuzi huo.

Kwamba kabla ya kuvunja mkataba, alitakiwa kwanza kupeleka maombi Yanga ya kutaka kuvunja mkataba na kueleza sababu za kufanya hivyo. Fei Toto hakufuata utaratibu huu, yeye alilipa aliyoiita fidia, kisha akaandika barua ya kuvunja mkataba. Hii haikubaliki.

Kwamba muda wa kuvunja mkataba haukuwa sahihi, mkataba hauvunjwi katikati ya msimu, labda kuwe na sababu maalum, lakini siyo za kutokuwa na



Fei Toto

mahaba na timu, au kupata timu nyingine. Mikataba inayovunjwa kwa kupata timu nyingine, huvunjwa kwa makubaliano na lazima timu anayotaka kwenda mchezaji, iombe ruhusa kutoka kwa klabu yake aliyu na mkataba nayo.

Kwamba madai ya Fei ya kuvunja mkataba, hayatokani na Yanga kukiuka makubaliano kwenye mkataba, wala yeye kupata majeraha, wala ubaguzi wa rangi, wala unyanyasaji wowote au mazingira magumu katika utekelezaji wa kazi yake, hivyo, FIFA hawawezi kukubali upuuzi na kuvunja mkataba kirahisi.

Kwamba Feisal kukimbia mazungumzo na Yanga ni kujichelewesha tu, kwa sababu, kawaida ya FIFA ni kutaka mchezaji aacheze ili kulinda kipaji chake, hivyo wakati wanaandelea kushughulikia kesi yake, watamwambia arudi klabuni kwake akacheze, mpaka shauri lake litakapopata uamuzi.

Kwamba Feisal akipeleka kesi FIFA na ikabainika kuna klabu ilimshawishi kuvunja mkataba, uwezekano wa FIFA kuifungia klabu hiyo kusajili misimu miwili mpaka mitatu ni mkubwa na hata Feisal mwenyewe anaweza kufungiwa na FIFA.

Mwandishi ni mbobezi kwenye uchambuzi wa soka.

Sugunyo ya Mandonga ‘yaua’ Kenya

Na Shabaan LULELA

NGUMI 73 zenye kasi na uzito za bondia kutoka Tanzania, Karim Said, almaarufu – Mandonga usiku wa kuamkia leo, zilitosha kumsimamisha mwanamasumbwi wa Kenya, Daniel Wanyonyi baada ya kusalimu amri na kuacha kuendelea na pambano.

Katika raundi ya tano, Wanyonyi alionekana kuchoka zaidi na kuishiwa ‘pumzi’ hivyo kuomba kutoendelea na raundi iliyokuwa inafuata ya mchezo huo wa ndondi uliofanyika kwenye ukumbi wa KICC, jijini Nairobi, Kenya.

Kabla ya pambano hilo la raundi 10, ambalo lilihudhuriwa na idadi kubwa ya watazamaji na mashabiki, Mandonga, maarufu pia kwa jina la Mtu Kazi, alitamba “kumchakaza” mpinzani wake kwa ngumi aliyoitia Sugunyo.

Mandonga alitamba kwamba ngumi hiyo ya Sugunyo iliyotoka Ukraine, kwenye mabomu, “itafanya kweli na Wanyonyi ajiandae kufa.”

Raundi ya kwanza ya mchezo ilianza kwa mabondia wote kusomana kimchezo; wakijitahidi kukwepa ngumi huku wakijikinga vilivyo, hivyo kumalizika bila kuwa na ‘mvuto wa piga nikupige.’

Hata hivyo, raundi ya pili na ile ya tatu, Wanyonyi alionyesha makeke na uzoefu wake akiwa ulingoni kwa kumpelekea ngumi kadhaa Mandonga, ambaye alionekana kupepesuka, lakini uwezo wake wa kukwepa ulimuokoa baadhi ya ngumi hadi kumalizika kwa raundi hiyo.

Raundi ya tano ilionyesha uwezo wa Sugunyo, ambapo Mandonga alimshambulia mpinzani wake kwa ngumi 11 mfululizo ambazo tano kati yake zilimpata vyema usoni Wanyonyi. Baada ya mapumziko, bondia huyo kutoka Nairobi, alikataa kuendelea na pambano hivyo, mwamuzi kumtangaza Mandonga kuwa mshindi wa TKO.



Karim Mandonga

Mandonga atacheza na Wanyonyi ambaye hayupo ‘active’ kwenye ndondi, mara ya mwisho alipigwa kwa Technical Knock Out (TKO) na Abdallah Pazi (Dullah Mbabe).

Wanyonyi licha ya kupoteza mchezo huo, rekodi zinaonyesha kuwa ana uzoefu mkubwa dhidi ya mpinzani wake, na kushindwa kwake kunaenezwa na wataalamu wa mchezo huo kuwa ni “kupumzika kwa muda na kushindwa kufanya mazoezi. Wanyonyi, tangu Februari 2021 hajapanda ulingoni baada ya kuchakazwa na Dullah Mbabe wa Tanzania.

Wanyonyi, ukiiondoa pambano la jana, bado ni mzoefu akiwa amepigana mapambano 43, ameshinda mara 27 amepigwa mara 14 na kutoka sare mara mbili.

Rekodi za Mandonga zinaonyesha kuwa amekuwa akipanda kwa ubora duniani, akiwa anashikilia nafasu ya 446 – kwa uzito wa kati na kwamba ni bondia wa tano kwa ubora nchini Tanzania kwa sasa.



Mikono ya mwanamama anayefanya kazi shamba la mikorosho huko maeneo ya Kilifi, Kenya. Vidole vyake vimeungua kwa kufanya kazi ya kuchambua na kubangua korosho bila kutumia vifaa vya kumkinga na madhara hayo. Mama huyo hulipwa Sh. 600 kwa siku (Sh. 30 ya Kenya). Picha hii imepigwa na Daniel Faraja.

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

